MAHUBIRI N°14: UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU

(*Jumapili asubuhi, aprili 2003 pa Locodjro, Abidjan - Côte d'Ivoire / www.matth25v6.org*)

Vema, Bwana awabariki! Ningependa tuimbe huo wimbo zuri wa zamani: Bwana rudisha siku hizo nzuri! [Kusanyiko wanaimba]

Kabla tuingie katika lengo, muniruhusu niseme hivi: hakuna hapa shauri la wazee. Na kama italazimu siku moja iwe, ni kwa mambo ya mwili tu. Mipango za muhimu sana hasa za kiroho inabidi ziwekwe kwa kazi ya karama za Roho au kwa watu waliojazwa na Roho kwa maana hekima ya mwanadamu haipaswe kuongoza Kanisa.

Napenda pia kugusia kidogo swali moja katika kitabu cha Danieli… Kichwa cha zahabu cha Danieli 2 na simba ya Dan. 7 ni ufalme wa Babiloni ulio tawala dunia tangu 606 mpaka 538. Ninakumbusha kwamba Misri pia ilikuwa utawalo kubwa wa dunia tangu 1600 mpaka 1200 kabla Yesu-Kristo. Vema, kifua na mikono ya feza ya Dan.2 na Dubu ya Dan.7 ni mfano wa ufalme wa Medi na Persi. Tumbo na paja ya shaba na chui ni ufalme wa Ugiriki ulimwenguni. Chuma ni Roma ya magharibi, Vatikani, na potopoto ni Roma ya mashariki, kanisa orthodoxi iliyo jitenga na Roma katika mwaka wa 1054. Anaonekana katika Ufu.11:7. Tunakuta vile vile Roma katika sura 7 ya Danieli, nyama ya nne na tunaona kwamba kwake kuna nyayo za wanyama wengine, Ufu.13:2.

Twende sasa kwa Danieli 9:23-27. Ni juma 70 za amani na za agano ya Mungu pamoja na Israeli, siyo pamoja na mataifa lakini pamoja na Israeli. Shairi la 25: tangu Nehemia 2 kwa mwaka 455 kabla Yesu-Kristo mpaka kwa ubatizo wa Yesu, *"kuna majuma 7 Na majuma 62"* kama inavyo semwa na wamoja wamoja. Kwa hivyo inafanya majuma 69 ambayo ni miaka 483 na inabaki juma moja ya unabii maana yake miaka saba. Yesu-Kristo alifanya kazi ya huduma yake muda wa nusu ya juma, miaka tatu na nusu na katikati ya juma zabihu itasimamishwa kwa Israeli ili Mungu awageukie mataifa. Kunabaki sasa nusu ya juma kwa Israeli mahali watapokea tena Masiya kupitia Elia na Musa. Baada ya hapo, watu wa Kaisari, Roma aliingia na kuharibu Yerusalema. Kisha Roma akafanya pia agano pamoja na wengi maana yake mataifa katika juma ya nyakati za Kanisa na ile ni kupitia kanisa katolika. Inampasa Mungu kutumika na mataifa kwa muda wa nyakati saba, kisha tena baadae pamoja na kabila kumi na mbili za Israeli. Kama mukikumbuka, wakati wa kuzidisha mikate kule Betesaida, walikusanya vitunga kumi na mbili, na wakati ya kuzidisha [mikate] mara ya pili, walikusanya ndegea saba. Ni matendo ya unabii kwa maandalio ya mambo yatakayokuja. Tayari mumekwisha kujua mambo yote haya. Mungu akiruhusu siku moja nitafasiria sura ya kwanza ya Ezekieli. Vema zaidi, turudi sasa kwa lengo letu. Roho Mtakatifu ni Mungu mwenyewe na basi yeye hawezi kuja juu ya kitu kingine mbalimbali na Neno. Roho Mtakatifu hawezi kamwe kuja juu ya mtu aliye na mafundisho ya uwongo. Na tunatambua kufwatana na Biblia kwamba Roho hatangulii Neno. Ilikuwa hivi kwa Kornelio. Kila roho ina msingi ya mvuto wake. Yesu alikuwa Neno na basi Roho aliweza kuja juu yake. Vilevile Neno lenyewe linakuja tu kwa nabii. Yesu alikuwa Neno na akaja kwa Yoane, nabii. Ni ile ndio makao yake. Tangu unapo kuwa na kitabu cha uchawi, [hapo] unachukua pepo moja. Unapoamini kwamba wafu wanahusiana nawe, [hapo] una mapepo za uchawi. Nyuma ya kila imani, nyuma ya kila fundisho la uwongo kuna pepo moja. Basi kusoma Horoscope ni vibaya pia kama uzinifu! Kuwa na kitabu cha uchawi ni kama kuvaa hirizi. Kabla ya kuja kwa Bwana, kwa utafiti wa mambo isiyo ya kawaida na vitu vya hapa chini, watu walifanya agano za aina yote pamoja na mapepo za uchawi, orodha za uchawi, ésotérisme, numérologie, astrologie,... na inakupasa kuwa na mwenendo gani unapo kuja kwa Bwana. Je! Inakubidi kuwapa watu vile vitabu vya uchawi wala kuvitupa? Biblia inasema *"wengi ya walio jitoa kwa mambo ya kuvutia, wakaleta vitabu vyao na kuvichoma mbele ya wote"* Matendo 19:19. Kwa nini? Hauwezi kuwa na hivyo vitabu na vyombo hivyo juu yako na kumuomba Mungu akupe Roho wake! Kuna mapepo nyuma ya yote munayo yaona na inawabidi kufanya matendo ya kuonekana. Hamuruhusiwi kumupa mtu zawadi ya vitu munavyo vijua kuwa vibaya. Kama kitu moja si kizuri kwako, sababu gani utakipatia jirani yako hata ikiwa anakitamani? Hamuruhusiwi kuwapa zile kaseti, vitabu na vingine munapo jua kwamba kuna maroho nyuma ya vitu vile! Kuna upako nyuma ya watu wale, zile kaseti, vile vitabu,… iwe katika dunia wala ndani ya makanisa. Musiguse tena biblia Louis Segond, Thompson, Scofield,… ilikuwa vema mpaka wakati moja lakini sasa Roho ya unabii inawakataza! Muviachie wana wa Shetani, hamuwezi kuwa navyo tena na kuwa na Roho Mtakatifu pamoja! Ninaisema kwa jina la Bwana Yesu-Kristo! Yote inatoka kwa mambo isiyo ya kawaida ndiyo maana munalazimishwa kujitenga navyo.

Sasa kumbukeni kwamba shetani anaweza kufanya jambo njema hata kusema kweli, ndio maana watu wanamfwata nyuma. Kwetu sisi ni uwongo. Mchawi au mulozi anaweza kuangushwa na shetani ndani ya ukristo na kuanza kueleza zoezi, tafsiri iitwayo ujanja wa shetani. Ninawaarifu juu ya mambo yale. Kwa hiyo, wandugu walinileta vitabu ambavyo kati yake ni "ultime assaut (mwisho ya ushambulizi)" ya Rick Joyner, vitabu vya Jean Schwab. Vitabu vyote vyengi hivyo, barua, kaseti, ni lazima vipite motoni. Kuna vilivyo vya Dion Robert, J-B. Nielbien, T.L.Osborn, Rebecca Brown, Yonggi Cho,… nita vichoma hazarani kwa wakati unaofaa. Ni kwa ajili ya vitu vyote hivyo ndio maana Mungu haleti Roho wake kwa sababu watu hawatambui hata kidogo tofauti kati ya njema na lisilo njema. Neno la Mungu inaomba kutengana kabisa na vitu hivi! Hauwezi kusoma Jean Schwab na baada ya hayo kuomba ubatizo wa Roho Mtakatifu. Inayo tupasa, ni kuacha tupu viriba vyetu. Math.9:17: *"mvinyo mpya haiwekwi katika viriba vya zamani"*. Ninapo sema kitu fulani ni kibaya, usiseme: " katika redio fulani ya kikristo kuna vipindi vinavyo jenga, ndani yake hakuna kilicho kibaya ". ukipenda kuifanya, uifanye na sababu ngumu mbele ya Mungu, lakini ni uasi tu.

Vema sana, kumbukeni ya kuwa mtu akiwa na pepo, ni ile roho inayo chunguza matendo yake hata yaliyo mema. Kwa mfano, siku kuhani mkatolika ataandika kitabu kwa kusema kwamba ubatizo ni kwa jina la Yesu-Kristo, tunajua ya kama ni ujanja wa Shetani. Siku mtu wa kusanyiko la miungu au mubatisti atatoa kaseti nzuri ya nyimbo za kusifu, hatuta husika nayo. Ni ule ule upako ndio ulimupa hayo! Kaseti hizo ni za hatari kama zile za Elvis Presley na za Madona. Musijitafutie mapepo! Na kujua maneno haya inaonekana kuwa ya lazima. Ninawanenea kwa jina la Bwana, musiguse vitu vile hata kidogo! Muna heri kama mimi si kikwazo wala fazaiko kwenu. Juweni kwamba mitume hawakumfwata Yesu kwa sababu walielewa vizuri masemi ya Yesu. Yesu aliposema *"asiye kula mwili wangu na kunywa damu yangu…"*, mitume hawakujua maana yake ni nini

lakini walifwata kwa kuwa walikuwa na ufunuo wa Yesu ni nani. Munaona? Kama munaamini kwamba ni Mungu aliye nizungumzia tarehe 24 aprili 1993 halafu muamini tu. Lakini maneno yote haya ni nini? Kujitenga kabisa na mambo yoye! Ufu.12:14 *"... mbali na uso wa nyoka"*. Hata kama kitabu fulani au kaseti fulani ni zuri, mujitenge mbali nayo! Kama muna vitu vile, mwachane navyo! Je! Munalazimishwa kusoma vitabu vile? Munalazimishwa kusikiliza zile kaseti wala redio ziitwazo za kikristo? Sababu gani? Musidanganywe kwani siyo roho zuri inayo wasukuma kwa vitu hivi! Kama unaweza tena kuona jambo nzuri katika zile redio na televisheni halafu huja elewa bado. Kama ungeliambiwa: *"Kuja uone mchawi mmoja anaye sema kweli!"*, je! Ungekwenda? Kama huwezi, halafu sababu gani utakwenda katika ibada za makanisa hayo? Na kama mtu akikushauri ufundi wa « astrologie» kwa kufaulu hapa duniani, je utaikubali? Halafu sababu gani unasoma hivyo vitabu vya ukombozi na vingine? Kwa mfano kama kuhani wala nabii fulani au mwinjilisti akiandika kitabu cha ukombozi na hapo kwa kukosa kutambua ukaisoma, neno gani la uzima unapokea ambalo Mungu atasibitisha na miujiza munayo tafuta? Wao na vitabu vyao ni vyombo mikononi mwa Shetani. Usiseme kwamba alipoanza ilikuwa ni Mungu! Hapana! Iwe ndani ya zile makanisa wala ndani ya wale wanao jidai kuwa watu wa Mungu, ni Shetani jana, leo hata milele! [*Kusanyiko linasema: Amina!]*. Tazama mti wa ndimo-tamu, mti wa mandarina, mti wa pamplemuse au mti wa ndimo-chungu inapoota, ni kile ilichokuwa mwanzoni ndicho itafunua kwa mwisho. Ndio maana katika Math.13:24-30, Yesu aliwaambia waache kwanza… Na kwa mwisho, tunawaona wakifungwa kwa ganda kwa kuchomwa: ganda batisti, ganda kusanyiko la miungu, foursquare,… hawana mafundisho moja lakini wanaungana katika miungano na shirikisho za makanisa. Ni kama zizi linalo beberu, mbuzi, nguruwe, mbwa, ngombe, nguruwe…Ngombe zinalia ouuuhh!! Nguruwe zinalia gr!gr!gr! wabatisti wanalia hivi, wametodisti wanalia namna ingine! Mbuzi wanalia…[cheko]! Inafaa uwe mtoto wa ibilisi kwa kubaki ndani ya zile makanisa! Hata wao ni wanyofu, watakwenda jehanama, nimewaambia ninyi! Biblia inasema katika Ufu.13:8 kwamba majina yao hayakuandikwa katika kitabu cha uzima!... Kumbuka Ufu.6, mihuri, mpinga Kristo alipo toka, ungeweza kufikili kwamba alikuwa ni Yesu lakini ni nyuma alipo badilisha farasi ndipo ilionekana kwamba alikuwa Shetani. Munaona? Alikuwa mweupe kabisa, udanganyifu. Na ni kile walicho ndicho kinajifunua baadae! Basi usiseme kwamba mwanzoni ilikuwa ni Mungu. Achana na wanamemba wa makanisa zile! Ni makaburi na ni watu wenyi wazimu ndio wanao zoea makaburi. Sitaki kuwahamakia lakini sitaki mlimaji asiye jua kusoma aje kanisani kuabudu ile ile pepo ya maji chafu anayo ikimbia.

Biblia katika Ufu.17: inasema kwamba watoto wa shetani watashangaa… lakini sisi, tunajua kwamba watakwenda motoni! Musipatane na waamini wao kwa kuhukumu wakatolika na wapagani kwani sisi si wamoja [nao]. Hata kama wanabatiza kwa jina la Yesu, wanafukuza mapepo, wanasema kwa lugha… Wakikueleza ndoto, usiseme kitu! Kama itabidi Mungu awazungumzie, ni kuwaonyesha njia ya Kweli. Na kwa kutafsiri ndoto, inafaa utambue kwanza roho iliyo zungumza ndipo unapaswa kupata tafsiri ya Mungu mwenyewe. Na kwa kutafsiri ndoto inabidi uwe nabii. Soma Mwanzo 41 na Dan 2.

Haifai kuruhusu watu waje kueleza ndoto kwa mazabahu. Mungu alileta karama 9 kwa ujenzi ya wote. Kile Mungu anacho taka kuzungumzia kanisa, ataisema mara moja. Na kama ndoto ilitumwa kwa kanisa, Mungu mwenyewe ataishughulikia. Kwa mwaka 1994, karibu mwisho wa mwaka, nilipata ndoto na juma moja baadae, katika mkutano ya kipekee uitwao mkutano ya uamsho, mbele ya watu zaidi ya mia moja, Roho akashuka juu ya mchungaji aliye jiunga nasi na kumuongoza mpaka kwangu na kusema hivi: *"Bwana anasema hivi: nilicho kuambia, simama na ukieleze sasa! "*. Roho akaja juu yangu na kutia maneno kinywani mwangu, nilisema nilicho ona. Niliona mashemasi wawili wakishika kusanyiko kama mwanamke msichana mrembo zaidi sana lakini kahaba kwa kumusonga shingoni. Kila mara alitafuta mali ya dunia alizo zipata lakini yuko tasa, mwisho wake ulikuwa mbovu baada ya kufa kwa mume wake.

Na kwa kumaliza, jueni kwamba mahali Kelele ya katikati ya usiku imefika, kama kusanyiko za ujumbe wa jioni wanasema kwamba walipokea Roho mtakatifu, ni uwongo! Hata kama wanasema waliipata zamani, ni uwongo! Kama ni hivi wangeliweza kukubali Kelele ya katikati ya usiku. Ni roho ya uchawi walio ipokea hata kama ni katika Krefeld au Branham-Tabernacle. Hata kama wana karama na yote inayo jifunua. Ninaisema kwa jina la Bwana Yesu. Wao ndio kahaba mzungu-nusu katika ono la tarehe 24 aprili 1993.

Kisha mahubiri haya, kila mtu anapaswa kujitambua hata kwa namna ya upekee unaweza kutambua ubatizo wa Roho Mtakatifu ilio Roho ya Neno la wakati na hiyo pamoja na karama zote za Roho na huduma kama inavyo semwa katika 1Kor.12. yote ni kwa utaratibu, Neno kisha Roho [inafwata]! Ndivyo ilivyo kuja kwa wayahudi, kwa wasamaria na kwa mataifa. Sisi ni tayari sasa na nilisema kwamba Malaika wa Bwana atajionyesha tena. Macho yenu yatamwona. Ninaitabiri. Musiwe na shaka hata kwa neno moja tu na musitwae kitu nje baada ya kujua Kweli, kitu ambacho kitawaondoa ubikira wenu. Ninapo sema kwamba wakati ya uumbaji mbinguni Mungu akasema: "Tumfanye malaika kwa mfano wetu…", ijapokuwa haiandikwe, ijapokuwa hamuielewi, muiamini tu. Hatari ninayo wahepusha ninyi pasipo kuchoka ni hamu ya ujuzi. Shabaha ya ujumbe huu siyo kuletea watu ujuzi mwingi lakini ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tusiisahau! Na mioyo zenu zisikubali kamwe kanisa ambalo limekufa na lililo la kawaida tu pasipo karama za Roho.

Lakini mambo yote haya ni nini? Wandugu, kufikia ukamilifu wakati ungali hai itatushurtisha mambo mengi! Mujue kwamba wafu katika Kristo, toka Paulo, wao ni katika kiwango moja cha Roho pamoja nasi tutakao kwenda katika kuchukuliwa! Je! Wao si mbali na hivyo vitabu, kaseti,… ninavyo wakataza ninyi kuvigusa? Wao si mbali na haya makanisa za uchawi? Ndio maana pia Mungu alitayarisha nafasi hii, hii jangwa na hii mahubiri ya Math.25:6 itakayo tutenga na yote kama inavyo andikwa katika Ufu.12:14 *"...mbali na uso wa shetani "* munaona? Kama vile wafu katika Kristo wamekatwa na dunia, ndivyo sisi tulio hai sharti tukatwe na dunia kwa namna fulani. Amina! Musa alikwenda jangwani kabla ya huduma yake, Yoane Mubatizaji alikwenda jangwani kabla ya huduma yake hata Yesu pia yeye mwenyewe. Jangwa ni kipindi cha faida kubwa kwa utakaso. Munakumbuka ono la pili: nilichukuliwa jangwani kupokea mana ya kiroho inayo shuka juu ya mawingu kama vile ilivyo kuwa jangwani pamoja na Musa. Ilikuwa ni mimi nanyi. Mulikuwa nami. Aleluya! Mbingu na nchi haviwezi kusemesha uwongo mambo tunayo kuwa tukiyaishi. Mutambue kwamba mfano wa mabikira kumi ni kwa mwisho ya huduma ya Yesu na utimilifu ya unabii za Mat.24. yote ile inapitika juu ya mlima wa mizeituni, nje ya Yerusalema na inatimia leo,

mwisho wa nyakati za Kanisa, nje ya mienendo zote hizo za kidini. Munaona? Mazabahu imerudishwa [sasa] munajua zambi ni nini na mukiwa wanyofu sioni tena kinachoweza kuzuia Roho kushuka. Asante Mungu.

Na tazama swali moja nililo liweka pembeni na ambalo nina… "*Ndugu Filipo, mtu anaweza kupoteza Wokovu?*" Haya, Wokovu ni uzima wa milele na namna moja tu ya uzima wa milele iliyo, ni Mungu mwenyewe maana yake Roho Mtakatifu. Kama basi ni Roho Mtakatifu wa kweli ndiye alikuwa juu yako, hakika unaweza kwenda jehanama kama ile ubatizo ilifanyika tu katika roho yako. Munaona? Roho anapo shuka, wamoja wanampokea katika nafsi; pale, wametiwa muhuri hata siku ya kukombolewa lakini wengine wanampokea tu katika roho kama Saulo, Balama na wengine. Munaona? Biblia inasema kwamba mvua inanyesha juu ya majani mazuri na juu ya majani mabaya. Japo, Roho mtakatifu ya kweli inayo nyesha juu ya majani mabaya haiyaokowi. Munaona? Ilikuwa tu katika roho! Lakini watoto wa Mungu wanapokea Roho katika nafsi kwani walipokea ufunuo ndani ya moyo kwa imani! Walipokea Neno moyoni! Munaona? Ni leo ndipo mambo yote yanatendeka. Ufunuo wa unabii unapaswa kwenda wima moyoni kwa imani. Lakini ukiupokea tu katika roho kwa akili yako, utapokea Roho… utapokea tu upako usiyo hakikisha wokovu wako wa milele. Sasa, kama mtu anakwambia: *"Tumeokolewa siyo kwa matendo lakini kwa neema… unaweza kunywa, kuvuta sigara, kufwata wanawake na kwenda paradiso!"*, ujitenge mbali naye na kama ndugu mmoja anaanza kusema maneno kama haya, afukuzwe toka Kanisa!

Tuombe ! Bwana Yesu-Kristo, Mwaminifu na wa Kweli, Kelele ya katikati ya usiku, ombi letu ni: Kuja Bwana Yesu! Ndugu Abou… aje sasa kwa kumaliza mkutano! Mungu ninaye mtumikia awabariki!

MAWASILIANO: Ndugu Filipo:+ 225-0252-0252 E-mail: kacou.philippe@yahoo.fr
Upate mahubiri katika site ya: www.matth25v6.org